

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ كَامَنُوا مِنْكُمْ وَعَكَلُوا الصَّدَقَاتِ لِيَسْتَخْلِفُنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَنْتُمْ تَعْمَلُونَ
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَمْ يَكُنْ لَّهُ بِهِمْ أَثْقَلُ طَمْمٍ وَلَمْ يَكُنْ لَّهُمْ مِنْ بَعْدِ حَرْقَهِمْ أَنَّهُمْ
يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّاغِنُونَ

Tanzia ya Mbebaji Ulinganizi

[مِنَ الْمُؤْمِنِينَ رَجُلٌ صَدَقَوْا مَا عَاهَدُوا اللَّهُ عَلَيْهِ فَمِنْهُمْ مَنْ قُضِيَ نَحْبَهُ
وَمِنْهُمْ مَنْ يَنْتَظِرُ وَمَا يَنْلَوْ إِلَّا يَنْدِيلَ]

“Mionganini mwa Waumini wapo watu walio timiza waliyo ahidiana na Mwenyezi Mungu.
Baadhi yao wamekwisha kufa, na baadhi wanangojea, wala hawakubadilisha (ahadi) hata
kidogo.” [Al-Ahzab:23]
(Imetafsiriwa)

Kwa kuamini qadhaa ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir/Wilaya ya Jordan inaomboleza pamoja na Umma wa Kiislamu kwa jumla na watu wa Jordan hasa Shab wa Hizb ut Tahrir, mmoja wa waaminifu wake, wenye subira na wenye matumaini.

Ndugu mtukufu:

Ustadh Omar Faleh At-Tal (Abu Abdullah)

Aliyeaga dunia kwenda kwenye rehema za Mwenyezi Mungu Mtukufu jioni ya Jumapili, tarehe 25 Ramadhan 1444 H sawia na tarehe 16 Aprili 2023, akiwa na umri wa takriban miaka 70, ambayo alitumia katika kumtii Mwenyezi Mungu (swt) na kufanya kazi pamoja na Hizb ut Tahrir kuregesha tena maisha kamili ya Kiislamu kuititia kusimamisha Khilafah Rashida kwa njia ya Utume.

Na yeye, Mwenyezi Mungu amrehemu, alijunga na Hizb ut Tahrir katika ujana wake, akibeba mwito wa haki na kheri, akivumilia kwa subira mateso, kukamatwa na kufungwa jela kwa ajili yake. Aliingia kwenye magereza ya madhalimu mara 16 kati ya hukumu za dhulma na kukamatwa kwa dhulma, akitarajia malipo kwa Mwenyezi Mungu, akitegemea ushindi Wake, Azza wa Jal. Aliteswa katika kifungo cha upweke na aliadhibiwa sana, na yeye, Mwenyezi Mungu amrehemu, alibaki imara juu ya haki anayoibeba, akikaidi kwa wazi.

Mji wa Irbid unashuhudia kwamba alikuwa shujaa wa misikiti, na sisi hatumsifu yeyote mbele ya Mwenyezi Mungu. Hakuacha msikitini wowote bila ya kutangaza haki ndani yake kwa sauti yake ya kuvuma. Hakuogopa lawama ya mwenye kulaumu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na alitoa wito wa kuregeshwa upya kwa maisha ya Kiislamu na kuasiwiwa kwa Dola ya Khilafah Rashida.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu amrehemu maiti wetu, maiti wa Ummah, kwa rehema zake, na ampokee kwa mapokezi mema, na ayajaalie makaazi yake yawe ni Firdaws ya juu kabisa peponi pamoja na manabii, wakweli, mashahidi, watu wema na hao ndio marafiki wema, na kumlipa kwa niaba yetu, Uislamu na Waislamu malipo bora, kama ambavyo tunamuomba Yeye (swt) kwa ajili yetu na jamaa zake, subira, faraja, na rambirambi njema. Na hatusemi ila tu aliyotuamrisha Mwenyezi Mungu Mtukufu:

[الَّذِينَ إِذَا أَصَابَتْهُمْ مُصِيبَةٌ قَالُوا إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ]

“Wale ambaa ukiwasibu msiba husema: Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na kwake Yeye hakika tutarejea.” [Al-Baqarah:156].

Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir katika Wilayah Jordan